## Suala kuu la 4

## Funzo la Maisha

Ilikuwa siku ya Jumapili, mwendo wa thenashara. Machweo yalikuwa yakijongea. Ilivyokuwa desturi yake, Stephanie alikuwa ameketi katika chumba chake cha kusoma, akifanya kazi walizopewa darasani. Wakati huu, mwalimu wao aliwahitaji wasakure mtandaoni na kurekodi misimu mbalimbali katika kaunti yao.

Stephanie alibofya kitufe cha kuwashia kipakatalishi. Kilipowaka, mafaili yote yalionekana mara moja kwenye kiwambo. Kipakatalishi kile hakikuwa na namba ya siri. Stephanie alifurahi sana. Aliendelea kubofyabofya ovyo. Mara aliona ujumbe pembeni: "**Congratulations! You have won! Click here to claim your prize!**" Kando ya ujumbe ule kulikuwa na picha nzuri ya gari.

Moyo wa Stephanie ulizidi kupiga kwa furaha. Aliubofya ujumbe ule moja kwa moja bila kujiuliza maswali. Hata alipoulizwa atoe habari kumhusu, na umri wake, hakuogopa.

Stephanie aliulizwa atoe habari kuhusu mzazi wake, maana alikuwa na umri mdogo. Alitoa maelezo kumhusu baba yake, likiwamo jina lake na nambari ya simu. Ghafla, mtandao ule ulijifunga. Stephanie naye akaanza kujuta kuwa hakuzingatia msemo: tahadhari kabla ya hatari.

Stephanie aliendelea na kazi zake. Alisakura na kufungua gatuzi lake la Uasin Gishu, akaona orodha ya misimu: masika, vuli, kiangazi, kipupwe na mingine. Alifungua kila moja, akasoma huku akinakili maelezo kuhusu msimu huo daftarini. Alipomaliza, mwendo wa saa moja kasorobo, alifunga mtandao ule kisha akakifunga kipakatalishi.

Chajio kilikuwa tayari. Stephanie alijiunga na wazazi wake mezani. Simu ya Bwana Oduori, Baba Stephanie, ilitoa mlio wa kuashiria alikuwa amepokea ujumbe mfupi. Baada ya wao kushtaki njaa, Bwana Oduori aliusoma ujumbe ule. Ulitoka kwa benki yake na ulimwarifu kuwa kiasi cha shilingi laki moja kilikuwa kimetolewa kwenye akaunti yake. Bwana Oduori alipigwa na butwaa.

“Ni nani anaweza kuwa ametoa pesa hizi? Yaweza kuwa ni matapeli? Kama ni wao, wamepata wapi maelezo kunihusu?” Alijiuliza. Mara akapigia benki yake simu na kuwaagiza waifunge akaunti yake ili pesa zaidi zisitolewe.

Stephanie alikumbuka kuwa alikuwa ametoa habari zile. Alimjulisha babake!

“Labda wao ndio wameipora akaunti yangu. Lazima wawe ni matapeli!” Bwana Oduori alisema kwa masikitiko.

Stephanie alisikitishwa sana. Alijutia kujibu ujumbe kutoka kwa watu asiowajua mtandaoni. Pia, alijutia kitendo cha kutoa habari, kuhusu baba yake, kwa watu asiowajua. Yote tisa, kumi ni kwamba maji yakimwagika, hayazoleki. Alikuwa amepata funzo la maisha.



Kimeidhinishwa na KICD